
Reli na Matukio
Februari 04, 2019 Toleo Namba 11.

# TRC KUKARABATI MABEHEWA 700 YA MIZIGO NA ABIRIA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akimuelezea Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe maendeleo ya ukarabati wa Mabehewa alipotembelea Karakana ya TRC makao makuu Dar es Salaam hivi karibuni Januari 2019.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe aridhishwa na kasi ya ukarabati wa Mabehewa ya mizigo na abiria alipotembelea Karakana ya TRC Makao Makuu Dar es Salaam kukagua kazi ya Ukarabati wa Mabehewa ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa Ukarabati wa Mabehewa 700 ya mizigo na abiria, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa jumla ya Shilingi Bilioni 5 kwa Shirika la Reli Tanzania kwa ajili ya kukarabati Mabehewa 100 awamu ya kwanza kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Shirika kutoa Huduma za Usafiri wa Mizigo na Abiria, Januari 2019.

TRC Reli na Matukio
Februari 04, 2019 Toleo Namba 11.



# SHIRIKA LA RELI TANZANIA KUKARABATI MABEHEWA 700 YA MIGZIGO NA ABIRIA



Mafundi wakipaka rangi behewa la Mizigo ikiwa ni miongoni mwa hatua za mwisho za ukarabati wa Behewa katika Karakana ya TRC Makao Makuu hivi karibuni 2019.

Shirika la Reli Tanzania laendelea na mpango wa kukarabati jumla ya Mabehewa 700 ya mizigo na Abiria ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa Huduma ya Usafiri wa Mizigo na Abiria, Mabehewa 100 yatakarabatiwa kipindi cha awamu ya kwanza ambayo utekelezaji wake umeanza na mabehewa zaidi ya 20 yamekarabatiwa. Mpango wa ukarabati wa Mabehewa unakwenda sambamba na Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati – TIRP unaoendelea ukiwa na dhumuni la kuboresha miundombinu ya reli ya zamani (Meter Gauge Railway) kuweza kutoa huduma bora ya usafiri wa reli.



Behewa kabla ya Matengenezo




Behewa baada ya Matengenezo



Behewa kabla ya Matengenezo



Behewa baada ya Matengenezo

TRC Reli na Matukio
Februari 04, 2019 Toleo Namba 11.

# TRC YAENDELEA KUWANOA WATAKAOSIMAMIA MIFUMO MIPYA YA RELI YA KISASA - SGR



Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala kutoka TRC Bwana Elifadhili Solomon (wa pili kushoto) akifungua Darasa la tatu la awamu ya pili ya mafunzo maalum yanayoratibiwa na TRC ili kuandaa wataalam watakaosimamia Shughuli za Uendeshaji wa reli ya kisasa – SGR katika Darasa la mafunzo lililopo kambi ya SGR Ilala Shaurimoyo Dar es Salaam Februari 04, 2019.

Shirika la Reli Tanzania laendelea na mpango wa kutoa mafunzo ili kuandaa wataalam wazawa watakaosimamia Shughuli za uendeshaji wa Reli ya Kisasa - SGR baada ya kufungua Mafunzo ya wiki tano kwa Darasa la tatu la awamu ya pili kuhusu uendeshaji treni za umeme, ukarabati wa reli, mabehewa, vichwa vya treni, pamoja na mifumo ya umeme na mawasiliano, ufunguzi umefanyika katika Darasa la mafunzo lililopo kambi ya ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Ilala Shaurimoyo jijini Dar es Salaam Februari 04, 2019.



Washiriki wa Mafunzo ya Shughuli za Uendeshaji wa Reli ya Kisasa – SGR wakifuatilia kwa umakini mada kutoka kwa mmoja wa wakufunzi kutoka nchini Uturuki mara baada ya ufunguzi wa Darasa la tatu la awamu ya pili yanayoendeshwa na Shirika la Reli Tanzania pamoja na Kampuni ya Yapi Merkezi ili kuandaa wataalamu watakaosimamia Shughuli za Uendeshaji wa reli ya kisasa – SGR, katika Darasa lililopo kambi ya ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Ilala Shaurimoyo Dar es Salaam Februari 04, 2019.

# WENGINE 24 WAHITIMU MAFUNZO YA SGR NA KUPATA VYETI



Shirika la Reli Tanzania – TRC laendelea na mpango wa Mafunzo kwa ajili ya kuandaa wataalamu watakaosimamia Shughuli za Uendeshaji wa Reli ya Kisasa ikiwemo ukarabati wa miundombinu mipya ya reli, usimamizi wa mifumo mipya ya mawasiliana na umeme pamoja na uendeshaji wa treni za kisasa zinazotumia umeme, mpaka sasa awamu ya pili ya mafunzo kwa darasa la pili imekamilika mwishoni mwa mwezi Januari 2019.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Yapi Mekrezi Ndugu Fuat Kamel akikabidhi vyeti kwa mmoja wa wahitimu wa Mafunzo kuhusu Shughuli za Uendeshaji wa Reli ya Kisasa – SGR kwa Darasa la pili la awamu ya pili katika ukumbi wa mafunzo uliopo Kambi ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa Ilala Shaurimoyo jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2019.



Washiriki 24 wa Mafunzo ya Shughuli za Uendeshaji wa Reli ya Kisasa – SGR katika picha ya pamoja na Wakufunzi kutoka Uturuki, Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala wa TRC Ndugu Elifadhili Solomon na Mkurugenzi wa Kampuni ya Yapi MerKezi Ndugu Fuat Kamel na wasimamizi wa Mafunzo TRC wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti kwa washiriki 24 yaliyofanyika katika Kambi ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Ilala Dar es Salaam hivi karibuni 2019.

Reli na Matukio
Februari 04, 2019 Toleo Namba 11.

# TRC YAENDELEA NA JITIHADA ZA KUDHIBITI MAFURIKO KILOSA - GULWE




Kazi Ujenzi wa kingo kwa kutumia mawe yenye jumla ya Tani 71,450 ikiendelea eneo la Kilosa – Gulwe lenye urefu wa Kilometa 83 mwishoni mwa mwezi Januari 2019 ili kudhibiti athari za mafuriko ya Mto Mkondoa unaoathiri Huduma ya Usafiri wa reli mara kadhaa wakati wa mvua kubwa. Ukarabati wa miundombinu ya reli eneo la Kilosa - Gulwe umefikia 85%.



Sehemu ya Kingo ya mto Mkondoa ikiwa imewekewa uzio wa Mawe ili kuzuia maji yanayoweza kuathiri tuta la reli wakati wa Mafuriko yanayosababishwa na mvua kubwa.



Kazi ya kutengeneza kalavati ili kuhamisha kipande cha reli urefu wa KM 1.3 ikiendelea eneo la Kilosa - Gulwe kwa lengo la kukabiliana na Mafuriko ya mto Mkondoa hivi karibuni 2019.